


Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 01 Issue: 01 | December-2022

EAJK

# Maudhui Kuhusu Jinsia katika Nyimbo za Kampeni za Kisiasa katika Kaunti ya Bomet, Nchini Kenya

**Authors**
**Nancy Kones** [(1)]; **Abdulrahim Hussein Taib Ali** [(2)]; **Mayaka Gwachi** [(3)]
**Main author email:** konesnancy2013@gmail.com

**(1) Egerton University, Kenya; (2) Laikipia University, Kenya.**

**Cite this article in APA**
Kones, N., Ali, A. H. T., & Gwachi, M. (2022). Maudhui kuhusu jinsia katika nyimbo za kampeni za kisiasa katika kaunti ya Bomet, nchini Kenya. *Eastern Africa journal of Kiswahili, 1*(1), 76-83. https://doi.org/10.51317/eajk.v1i1.326

OPEN ACCESS A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 20.10.2022
Accepted: 22.11.2022
Published: 25.12.2022

**Scan this QR to read the paper online**

**Copyright**: ©2022 by the author(s). This article is an Open Access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-NC-SA 4.0).

**Ikisiri**
Utafiti huu ulishughulikia namna maudhui ya nyimbo za kampeni za kisiasa huwakilisha jinsia katika Kaunti ya Bomet nchini Kenya. Ulichunguza iwapo nyimbo zilisababisha kuchaguliwa kwa wanaume wengi kuliko wanawake. Lengo mahususi la utafiti huu lilikuwa kufasili namna maudhui ya nyimbo za kampeni za kisiasa huwakilisha jinsia. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Ubabedume. Huu ni utafiti wa kithamano mkabala wa kifasili. Nyimbo hamsini na mbili za kisiasa zilizorekodiwa katika kanda wakati wa kampeni zilikusanywa. Sampuli ya kimakusudi ilitumika kuteua nyimbo ishirini na mbili za kampeni za kisiasa zilizohusika na jinsia. Deta zilikusanywa kwa usikilizaji wa kanda za nyimbo pamoja na mwongozo wa maswali ya mahojiano. Mbinu ya ufasili wa deta ilitumika katika utafiti huu. Matokeo ya utafiti huu, yalibainisha kwamba nyimbo nyingi za kampeni za kisiasa zilitetea jinsia ya kiume. Nyimbo hizo zilipatia hadhi ya juu jinsia ya kiume kuliko ya kike. Mtafiti anapendekeza kwamba utafiti ufanywe kuhusu namna jinsia ya kike husawirika kupitia maongezi na majadiliano katika mikutano ya kampeni za kisiasa.

**Maneno muhimu:** Jinsia, Maudhui, nyimbo za kampeni za kisiasa

**UTANGULIZI**

Nyimbo ni njia moja ya mawasiliano katika jamii. Nchini Kenya, nyimbo za kampeni za kisiasa hutumika wakati wa uchaguzi wa rais, magavana, maseneta, wabunge, wawakilishi wa wanawake na wajumbe wa wadi. Wasanii hubuni nyimbo za kuvisifu vyama na wagombezi wenyewe. Riordan (2007) anaeleza kwamba kuna hisi zenye nguvu zinazoambatana na nyimbo za kisiasa. Nyimbo hizo zina uwezo wa kuwasilisha ujumbe wa siasa. Utafiti ulichunguza iwapo viashiria vya jinsia katika nyimbo zilisababisha kuchaguliwa kwa wanaume wengi kuliko wanawake. Vilevile, utafiti ulimakinika kuchunguza jinsi gani jinsia iliwakilishwa katika nyimbo hizo na namna zilichangia wanaume ama wanawake kuchaguliwa.

Smith (2012) anaeleza kwamba kabla ya wanasiasa kuwahutubia watu katika mikutano ya kisiasa, huwachangamsha kwa nyimbo na ngoma za kuvutia kwa minajili ya kuwasilisha ujumbe wa kisiasa. Hali ya jinsia ni kikwazo kikuu katika nyanja zote za maisha ya Marekani. Hili ni jambo lililogundulika katika uchaguzi wa rais mwaka wa 2008. Utafiti wa 'National Women's History Museum' Marekani unaonyesha kwamba wanawake thelathini na watano wamewahi kuwania kiti cha urais lakini hakuna aliyechaguliwa.

Wafula na Njogu (2007) wanaeleza kuwa nyimbo na siasa katika nchi za Afrika Mashariki huleta pamoja habari muhimu kuhusu nyimbo na siasa za eneo lenyewe na pande nyinginezo. Wanatufahamisha kwamba maneno yanayotunga nyimbo yalichunguza mambo yapasayo binadamu. Mambo haya ni kama elimu ya sayansi ya ulimwengu pamoja na uasili na maendeleo yake, maono ya ulimwengu, daraja na uhusiano wa jinsia, tafsiri ya thamani ya siasa na mazoezi mengine ya kisiasa, kijamii na kiuchumi, hata kama yanachangamsha hadhira. Licha ya nyimbo kuwa nzuri, pia ni vyombo muhimu vya kuchunguzia namna matukio ya kisiasa na kijamii huendelezwa na kueleweka na raia.

Uchaguzi mkuu wa 1992 nchini Kenya, Hayati Daniel Arap Moi alishinda na Marehemu Kenneth Matiba alichukua nafasi ya pili. Hakukuwa na mwanamke mgombezi aliyewania kiti hicho. Nyimbo za kampeni za kisiasa hazikupatikana. Uchaguzi mkuu wa 1997, Hayati Daniel Arap Moi aliongoza na Hayati Mwai Kibaki alikuwa wa pili. Charity Ngilu kama mwanamke wa kwanza nchini Kenya na katika Afrika Mashariki, alikuwa wa tano (DDDG, 1998). Marehemu Waangari Maathai alikuwa namba kumi na tatu. Uchaguzi wa 2007, mshindi alikuwa Hayati Mwai Kibaki na wa pili alikuwa Raila Odinga. Nazlin Umar alikuwa wa sita (IEBC). Uchaguzi wa 2013 Uhuru Kenyatta aliongoza na Raila Odinga alikuwa wa pili. Martha Karua, kwa wagombezi wanane, alikuwa wa sita (Commonwealth Observer Group, 2013). Uchaguzi wa 2017, Uhuru Kenyatta alikuwa wa kwanza akifuatwa na Raila Odinga. Magavana wa kike watatu walichaguliwa kwa mara ya kwanza ambao ni Charity Ngilu, Ann Waiguru na Marehemu Dkt. Joyce Laboso.

Kabila la Kalenjin hujumlisha wanawake na watoto kuwa sawa. Kuambatana na wazo hili, wanaume huona wanawake kama hawawezi kuwa viongozi. Wanawake wameshawishiwa na wanaume kuwa wanawake wenyewe hawana uwezo wa kuongoza. Kwa hivyo, wanawake wagombezi hudharauliwa na wanawake wenzao. Kuna madai kuwa wnawake wanaweza kuchaguliwa iwapo wanagombea kiti katika chama maarufu kinachoongozwa na mwanaume aliye na ushawishi mkubwa. Marehemu Kipchamba alieleza katika wimbo wake kuwa gari linapokimbia, hakuna wakati magurudumu ya nyuma yanaweza kufikia ya mbele daima. Mtafiti alizichanganua nyimbo za kampeni za kisiasa zilizo na misimamo na mielekeo kama hii.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

**Maudhui ya Nyimbo za Kampeni za Kisiasa Kuhusu Jinsia**

Kwa mujibu wa Sengo na Kiango (1973), fasihi simulizi ni sanaa ya lugha inayofungamanishwa na maisha ya binadamu katika jamii. Nyimbo za kisiasa huimbwa kwenye shughuli za kisiasa kwa azma ya kuelewesha, kuhamasisha, kubeza na kutumbuiza kwenye sherehe. Demokrasia ya muziki inawawezesha wagombezi wa kisiasa kuleta tofauti kubwa katika matokeo ya uchaguzi. Hali halisi husawirika katika nyimbo za kampeni za kisiasa. Jambo hili limedhihirika katika utafiti huu.

**Mgawanyo wa Mamlaka**

Msanii mmoja aitwaye Jeremiah Kosgei aliwapigia debe Uhuru Kenyatta na naibu wake William Ruto wakati wa kampeni za kisiasa za 2017. Katika sehemu ya wimbo huu, Ruto alitumwa apeleke Uhuru

atakaswe na wazee wa kiume wa Kalenjin apate kulinda nchi ya Kenya akifanikiwa. Uhuru alifananishwa na Daudi mwana wa Jesse katika Biblia ambaye alikuwa mfalme wa maajabu aliyetenda makuu Uyaudi. Utawala wa jinsia ya kiume pekee ulisawirika. Connel (1983) anaeleza kwamba ubabedume sio namna wanaume wenye nguvu hujidhihirisha kwa jamii, bali ni njia ya kuhifadhi nguvu yao na ndio maana idadi ya wanaume wanahamasishwa kuunga mkono ubabedume huo kwa sababu unawafaidi. Rejea sehemu ya wimbo huo.

*Kokiyokten Samoei Arap Ruto.*
*Asiimutwech Uhuru konyo Kapkatet.*
*Si kikochin* ***mwaita*** *nebo Kalenjin.*
*Kou weritab Jesse nemi Bible.*
*Si koribwech emet.*
*Tunakutuma Samoei Arap Ruto.*
*Utuletee Uhuru aje nyumbani Kapkatet.*
*Ili tumpatie* ***mafuta*** *ya Kalenjin.*
*Kama mwana wa Jesse katika Biblia.*
*Yeye apate kutulindia nchi*

Kuna wasanii waliojiita Shuttle Sisters ambao walimpigia debe Ruto akiwa katika chama cha United Republican. Alikuwa akigombea kiti cha naibu wa rais mwaka wa 2013. Ruto, akiwa mwanaume, alisifika kama shujaa aliyejitahidi kuunda chama cha URP. Vilevile, ilielezwa kwamba yeye ni maarufu kote nchini. Anaombewa Mungu amwezeshe yeye wakati mmoja aongoze nchi ya Kenya akifuata nyayo za Mstaafu Hayati Rais Moi katika uongozi wake. Mstaafu Hayati Rais Moi alitawala nchi ya Kenya miaka ishirini na minne mfululizo hadi 2002 alipostaafu. Sehemu hii ya wimbo imebainisha nguvu na mamlaka yanayomilikiwa na jinsia ya kiume. Rejea sehemu ya wimbo huo.

Nyiganenyon Ruto koriborjige.
Kot iboru chamaitab URP.
Arap Ruto ko chorwetab chi tugul.
Mami bororiet Kenya ne moingen kainetab Samoei.
Kisaun kot indochi emenyon Kenya.
Ibur kou Baba Moi.

Shujaa Ruto umejitahidi.
Hadi ukaunda chama cha URP.
Arap Ruto ni rafiki ya kila mtu.
Hakuna jamii nchini Kenya isiyotambua jina la Samoei.
Sisi tunakuombea hadi uongoze nchi yetu ya Kenya.
Ukae kama Baba Moi.

Kikundi cha kina mama kinachoitwa CCM Women, yaani, wanawake kutoka Chama cha Mashinani, waliimba wimbo wenye mada 'Chama cha Mashinani'. Waimbaji hao walikisifu chama cha Mashinani kikiwa ndani ya Muungano wa National Super Alliance (NASA). Muungano huu uliongozwa na Raila Odinga na ulikuwa maarufu sana katika ugombezi wa kiti cha urais wakati wa uchaguzi wa kitaifa wa mwaka wa 2017. Chama cha Mashinani kilianzishwa na Isaac Ruto kutoka Kaunti Ndogo ya Chepalungu aliyekuwa akigombea kiti cha ugavana mwaka huo. Wasanii walimshukuru yeye kwa kuanzisha chama hicho na wakaeleza kwamba yeye ni fahali yao na hawakutaka aumizwe na yeyote. Walimwinua yeye wakisema kwamba wanampenda na yeye ni shujaa wao, shujaa mfano wa moto ambaye anatambulika katika nchi nzima ya Kenya. Walieleza kwamba kwa sababu ya maendeleo aliyofanya katika kaunti yao, hawezi kubadilishwa na kwamba angebaki kuwa kiongozi wao tena miaka mingine ijayo. Kupitia wimbo huu, uhodari wa jinsia ya kiume, ambao ni kielelezo chake cha mamlaka, umedhihirika. Richmond (1992) kama anavyonukuliwa na Aswani na wengine (2014), anafafanua kwamba jamii ni taasisi muhimu ambayo hujenga na kuratibu majukumu na shughuli za kijamii kiuana. Rejea sehemu ya wimbo huo.

Kongoi inye kirginyon Mashinani kityo.
Mokichomndoi kesilwech.
Kichome echek nyiganet.
Kongoi nyiganet neu mat.
Ne kikenai en Kenya.
Mokiwole kora.

Asante fahali yetu Mashinani pekee.
Haturuhusu aumizwe.
Tunampenda shujaa wetu.
Asante shujaa mfano wa moto.
Anayejulikana nchini Kenya.
Haibadilishwi tena

Msanii mmoja aitwaye Ben Bii alifahamisha kwamba kumekucha na watu waamke kwa sababu tunataka mabadiliko hususan katika siasa. Mada kuu yake ilikuwa 'Daktari Joyce Laboso' na mada ndogo ilikuwa 'Daktari Joyce Laboso Kaunti ya Bomet, mama na kazi.'

Alikuwa akimtetea mgombezi huyu wa kike katika kampeni za kisiasa za 2017.

*Bikab Bomet Kounti ong'et kakoech*
*emet.*
*Kogeger konyone walet.*
*Dr. Joyce Laboso ne koketach koik*
*Gavana.*
*Kiwole ra kele kiwole.*
*Kondoikyok ko kokelewen en chamaitab Jubilee.*
*Kokomwa kole kiwole.*
*Walaken ana komataikany si kewalin i.*
*Ni ko tugetab ng'omnotet o papa.*
*Watu wa Kaunti ya Bomet mwamke kumekucha.*
*Tumeona mabadiliko yakija*
*Tumepokea Dkt. Joyce Laboso kuwa Gavana.*
*Tutabadilisha wakati huu, tutabadilisha.*
*Viongozi wetu wamechaguliwa*
*katika Muungano wa Jubilee.*
*Wamesema tutabadilisha.*
*Badilika au ungoje ubadilishwe.*
*Hii ni sauti ya busara papa.*

Wasanii wengine walichanganya nyimbo za ulimwengu na za dini. Mfano mmoja ni msanii huyo aitwaye Ben Bii aliyemwunga mkono marehemu Dkt Laboso wakati wa kampeni za kisiasa mwaka 2017. Wakati alikuwa akiomba kuwe na mabadiliko ya uongozi, aliimba akidondoa maneno ya Bibilia. Aliyanukuu maneno hayo akielewa wazi kwamba neno la Mungu halitaweza kupingika kamwe. Alimwomba Mwenyezi Mungu mwenyewe ayalete mabadiliko hasa katika siasa inayopiganiwa na jinsia zote mbili. Alimwona marehemu Dkt. Laboso akiwa na uwezo wa kuleta maendeleo kwani mwanamke anaweza kupanda ngazi kiutawala. Rejea sehemu ya wimbo huo.

*Kimwa Kiptaiyat,'Osom si kekonok,*
*ocheng si onyoru, okongon si*
*keyotwok.'*
*Joyce Laboso ko Gavana nebo Bomet Kounti.*
***Chepyoset** o papa.*
*Ibuch Bomet kwo kotililit.*
*Yesu alisema, 'Mwombe halafu mpewe*
*mtafute halafu mpate na mgonge halafu mfunguliwe.'*
*Joyce Laboso ni gavana wa Kaunti ya Bomet.*
*Ni **mwanamke** o papa.*
*Fagia Bomet hadi ing'are*

Marion Chelang'at ni msanii aliyeeleza zaidi juu ya uongozi wa jinsia ya kike. Yeye pia alikuwa akimwunga mkono marehemu Dkt. Laboso awe gavana mwaka wa 2017. Alimdhihirishia kwamba alikuwa akipendezeka na kuhitajika sana katika kaunti. Ingawa watu wanataka maziwa, si lazima kuweko na ndume halafu maziwa yapatikane kwani kuna njia nyingine ya kuyapata. Hii ni wazi kwamba si lazima mwanamume aongoze na kwamba watu wanataka mabadiliko. Wanataka mwanamke apewe mamlaka ili aweze kutawala. Maclenness (1998) alieleza namna ambavyo masharti ya kihistoria na ya kitamaduni yanavyohalalisha mielekeo na mitazamo tofauti baina ya jinsia ya kike na ya kiume. Rejea sehemu ya wimbo huo.

*Omwochin **Chemaluk** chamat mising.*

*Ndandan kimoche chego, ko malazima*
***kirgit.***
*Kimoche tuguk che lelach.*
*Ongele kiwole en Bomenyon.*
*Gavana ko Joyce, kamenyon*
*korur bai.*
*Telel en sera che koimwa.*
*Mmwambie **Chemaluk** anapendezeka sana.*
*Ingawa tunataka maziwa, si lazima tuwe na **ndume.***
*Tunataka vitu vipya.*
*Tuseme tutageuza katika Bomet yetu.*
*Gavana ni Joyce, mama yetu mwenye*
*uwezo wa kulisha jamii.*
*Simama imara na sera zako ulizo nazo*

Kuna mwimbaji aitwaye Arumutik Kosgei ambaye alimtetea William Lesan aliyekuwa akiwania kiti cha useneta katika Kaunti ya Bomet. Katika kabila la Kalenjin wazee wa jinsia ya kiume huheshimika sana. Mwimbaji alieleza kwamba vijana walishauriwa na wazee hao kuchagua mgombezi aliyebobea katika masomo kuwa seneta wao. Hii ni njia moja ya kuukuza ubabedume kwa maana mwanaume amehusishwa na hadhi ya juu. Vilevile, hili ni dhihirisho la kuimarisha ngazi ya mamlaka kwa jinsia ya kiume. Rejea sehemu ya wimbo huo.

*Kokekonuge vijana kisib ng'alekab*
*boisiek.*
*Kegas ng'alekab bamong'o.*
*Si ketech Bomet Kounti ba kolili, komoche chito ne*
*somanat.*

*Profesa somananing'ung ko* ***sobunitab*** *Bomet Kaunti.*
*Si kotililit bororienyon en ng'omnotet.*
*Sisi vijana tumejitolea kufuata mawaidha ya wazee.*
*Tusikie mawaidha ya baba.*
*Tukitaka kujenga Kaunti ya Bomet hadi ing'are, tunahitaji mtaalamu.*
*Profesa masomo yako ni* ***sabuni*** *ya Kaunti ya Bomet.*
*Ili nchi yetu itakasike kielimu.*

Msanii alieleza kwamba Lesan ni mgombezi aliye shujaa na hawezi kushtuliwa wala kutingishika katika kazi yake. Angeweza kuwa mwangaza wa kaunti na kwa sababu ya ukarimu wake, angeichunga sahani ya wazee ili wanaume wengine wadogo waje wakailia siku za usoni. Msanii huyo alikiona kiti hiki kikiwa cha jinsia ya kiume kulingana na maelezo yake. Alieleza kwamba mgombezi alitarajiwa kukalia kiti cha useneta kwa njia ifaayo na muda wake ukiisha, awawachie wanaume wengine wadogo wa vizazi vingine vijavyo. Rejea sehemu ya wimbo huo.

*Si koribwech* ***kisienyon*** *bo kok.*
*Sinyon kwomisien murenjun chon mengech.*
*Profesa Lesan ko nyiganet.*
*Lesan, konyoljin ng'echeret.*
*En oyebindo ak nyiganatet ne itinye.*
*Ma kitisionin.*
*Seneta nenyon ko moitumtumokse.*
*Apate kutuchungia* ***sahani*** *yetu ya wazee.*
*Ili wanaume wale wengine wadogo wapate kuilia.*
*Profesa Lesan ni shujaa.*
*Lesan, kiti kimekufaa.*
*Kwa ukarimu na ujasiri ulio nao.*
*Huwezi ukatishwa.*
*Seneta wetu hawezi kutingishika.*

Msanii alimshauri mgombezi ajadiliane na wenyeji namna ya kuelekeza vijana katika mambo ya masomo, ukulima, afya na maendeleo kwa jumla. Alielezea umma kwamba Lesan alikuwa mwanaume aliyekuwa bingwa katika masomo na matibabu kwani shahada yake ya uzamifu ilikuwa kama fimbo iliyotumiwa na Musa katika Biblia. Musa aliyagonga maji ya Bahari Nyekundu na yakatawanyika halafu Wayaudi wakaweza kuvuka. Busara ambayo ingetumika na Lesan kama angefanikiwa ilimithilishwa na ya Musa kwani msanii alifafanua kwamba watu wangevukishwa, yaani, wangefaulu katika mambo yanayohitajika katika maisha kama vile ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Alitaja kwamba wakiwa na maendeleo kama hayo, wanaume wale wengine wangewaheshimu. Nguvu na mamlaka yanayomilikiwa na jinsia ya kiume yamesawirika katika wimbo huu.

Carrigan na wengine (1985:595) wanaeleza kwamba kipengele kikubwa cha kuangazia somo kwa wanaume, ni lengo kuhusu mabadiliko ya kisaikolojia ya kijinsia. Walisisitiza kuwa hayawezi kutenganishwa na mahusiano ya kijamii ambayo yanakuza na kujenga ubabedume. Maelezo hayo yanasawirika katika sehemu ya wimbo huo.

*Ong'alal ak bik ele kiribto barnotik ak keipto somanet.*
*Ak kerib emenyon ba kolele.*
*Somanet ko i chonjo.*
*Konyoiset ko i chonjo*
*Digrii ne itindoi ko kerge ok* ***kiroki*** *kibo Musa.*
*Kilondoi ra akechek.*
*Mjadiliane na wenyeji jinsi ya kutunza vijana na kuyaendeleza masomo.*
*Na kutunza nchi yetu hadi ing'are.*
*Kimasomo wewe ni bingwa.*
*Kimatibabu wewe ni bingwa.*
*Shahada ya masomo uliyo nayo ni kama* ***fimbo ile*** *ya Musa.*
*Sisi tutafaulu wakati huu.*

Richard Cheselet aliyekuwa akiwania kiti cha ubunge wa wadi, alipigiwa debe na msanii aitwaye Kachwes Rotich mwaka 2017. Aliwasihi wananchi wampigie kura tena kwa sababu ni mwanaume aliye na roho safi na hana ubaguzi wala ukabila. Matendo yake yameonekana wazi tangu awe kwenye kiti hicho 2013 kama vile kujenga barabara, shule na kuleta pesa ya serikali ya kusaidia wanafunzi shuleni. Maelezo ya msanii yamedhihirisha uwezo aliokuwa nao mgombezi katika kazi yake tangu 2013. Wimbo huu unaukuza ubabedume kulingana na jinsi ambavyo msanii aliwashawishi wapiga kura kumchagua tena mgombezi yule. Wanajamii huamini kwamba uongozi unamfaa mwanaume, jambo lililokolea kwenye akili zao. Rejea sehemu ya wimbo huo.

*Olewen chitugul Cheselet koik MCA kototen.*
*Chi ne mie mugulel.*
*Motinye ubaguzi ako motinye ukabila.*

*Barabarosiek ko miach, ng'alekab sugul, ak bursaries.*
*Bikab Olol Masani, ongeketyin*
*Cheselet.*
*Nyote mchague Cheselet awe MCA mara nyingi.*
*Ni mtu mwenye roho safi.*
*Mtu asiye na ubaguzi wala ukabila*
*Barabara ni nzuri, amejenga shule na ameleta*
*'bursaries.'*
*Watu wa Olol Masani, tumrudishe Cheselet kitini.*

Kachwes alimtetea Cheselet kupitia methali. Alieleza kwamba kuna mhenga aliyesema kuwa haifai mtu yeyote mwenye akili timamu kujikinga kwenye mti fulani kukiwa kunanyesha kisha mvua ikikoma, aukate mti huo. Alifahamisha kwamba yeyote aliye na ng'ombe ampatiaye maziwa mengi, asithubutu kumwacha na kujaribu kumtafuta ng'ombe mwingine tofauti asiyemjua. Ni afadhali aendelee kumkama yule yule amemzoea kuliko kumtafuta yule asiyemfahamu. Msanii alieleza hivi akiyafananisha na matendo mema ya Cheselet. Alimtetea akisema kuwa mgombezi anawapenda watoto, wazee na hata walemavu. Alimpatia moyo aendelee na uongozi uo huo wake mwema kama vile Musa alivyowaongoza Waisraeli namna inavyoelezwa katika Biblia. Wimbo huu ulikuwa ukiwashawishi wapiga kura wampigie tena mgombezi yule wa kiume. Jambo hili lilikuwa likiendeleza na kudumisha utawala wa jinsia ya kiume kama tulivyoelezwa na Connell (1987). Rejea sehemu ya wimbo huo.

*Kikamwa boiyon kole* ***meyumen sosur***
***ye moen iyeb.***
*Yon karibai teta ako igosu chego*
*Mhenga aliyesema* ***usijikinge katika 'sosur'***
***kukinyesha na kuukata mvua ikikoma.***
*Ukimfuga ng'ombe aliye na maziwa mengi*

*ko mebwat ile awalda asi awal butiot.*
*Cheselet kochome ne ming'in, ne kakoyosit*
*okot solomwet.*
*Ongeketyin we bikyok.*
*Indochin bikuk kou Musa we Richard Cheselet.*

*usifikirie ubadilishe upate mwingine tofauti.*
*Cheselet anampenda aliye mdogo,*
*aliyezeeka na hata mlemavu.*
*Tumrudishe tena kwenye kiti.*
*Waongoze watu wako kama Musa ewe Richard*
*Cheselet.*

Kupitia nyimbo zilizochanganuliwa na kufasiliwa, iligundulika kwamba utawala wa jinsia ya kiume umedumishwa na wa kike bado unajitafutia nafasi yake katika jamii. Jambo hili limelandana na namna ambavyo nadharia ya Ubabedume yaeleza kwamba nguvu na mamlaka yanamilikiwa na jinsia ya kiume kulingana na utamaduni wa jamii husika. Wasanii wengi wa jinsia ya kiume waliimba nyimbo za kampeni za kisiasa kuliko jinsia ya kike. Kulikuwa na waimbaji wa jinsia ya kiume waliopigia debe wagombezi wa jinsia zote mbili. Wagombezi wa jinsia ya kiume walikuwa wengi kuliko wa kike.

Nyimbo za kampeni za kisiasa ni za kuburudisha, kuelimisha, kuhamasisha, kushawishi, kuunganisha watu katika jamii na kuwashikamanisha wanachama wa chama fulani angalau chama chao cha kisiasa kipate kuwa na nguvu. Kila msanii alikuwa akimsifu mgombezi kwa njia ya kipekee, mgombezi awe wa jinsia ya kike au kiume. Wale waliodhihakiwa katika nyimbo ni wagombezi ambao wasanii hawakutaka kuwaunga mkono. Nyimbo kadhaa ziliwaelezea wananchi kuhusu nguvu za wagombezi kisiasa hususan kupitia sera zao. Wanachi waliahidiwa kwamba wangeletewa maendeleo makubwa kama vile kuletewa maji na umeme, kujengewa shule, hospitali na barabara, kuwalipia karo watoto wa wazazi wasiojiweza, kuwasaidia vijana kupata ajira, na kuwasaidia hata walemavu. Wasanii wengine waliwatetea wagombezi wengine wapigiwe kura tena kuambatana na kazi waliyowafanyia watu katika miaka mitano iliyopita. Waliotaka kugombea viti vya kisiasa hususan walikuwa wa jinsia ya kiume.

**MATOKEO**

Kupitia nyimbo hizo tunajifunza mambo mengi kwani wasanii wanapobuni nyimbo zao, huwa hawaendi nje ya utamaduni wa jamii zao katika mazingira wanamokulia (Mazrui & Syambo, 1992). Wasanii walieleza kuhusu nguvu za wagombezi kisiasa hasa kupitia sera zao. Wagombezi wengine wa kiume walitetewa na wasanii wawanie upya viti vya kisiasa. Nyimbo nyingi zilieleza kuhusu maendeleo kadhaa waliyofanya walipokuwa vitini. Hili ni jambo ambalo lingewashawishi wapiga kura wawapigie kura tena. Kulikuwa na wimbo mmoja ulioidhalilisha jinsia ya kike

kwa kueleza kwamba gari likiwa mbioni, magurudumu ya nyuma hukimbiza ya mbele na hayatafikia kamwe. Kulingana na msanii huyo, magurudumu ya mbele husimamia jinsia ya kiume na ya nyuma husimamia ya kike. Huu ni mwelekeo chanya kwa mwanaume na mwelekeo hasi kwa mwanamke.

Kupitia nyimbo za kampeni za kisiasa, wanaume hupewa nguvu, uwezo, hadhi ya juu na mamlaka kuliko wanawake. Uchendu (2005) anafafanua kwamba kisaikolojia, wanaume hutamani kuwa na mamlaka ya uamuzi, kuwalinda wanyonge, kuwa na msimamo thabiti, kuwa wa hadhi ya juu na kutoonyesha woga wowote. Mwanaume hutukuzwa zaidi kuliko wanawake katika jamii ya Kalenjin, jambo ambalo limewafanya wanawake wachache kuingia siasani. Sifa zifuatazo zinahusishwa na mwanaume kulingana na itikadi na utamaduni wa Kalenjin: Ni shujaa, ngao, moto, fahali, chuma, macho, baba, mtaalamu, mtetezi, mchungaji, mkarimu na yeye hana ubaguzi. Vilevile, nyimbo zilieleza kwamba yeye ni jasiri kwa sababu anaweza kumwua simba anayenguruma, anaweza kumwua simba kama simba anasimama, hashtuliwi kwa ngozi, anaweza kuinua mlima, analinda pembeni, akilia hutegewa masikio na akilia mali yanafika nyumbani. Yeye ni 'Kipkutuny' yaani, anawezana na maadui kwani anajua mbinu za kivita na hatishwi, hashtuliwi wala kutingishika. Yeye ni 'Koterkut' yaani, mtetezi wa watu hasa katika siasa. Yeye ni 'Kosilei' yaani, anashughulikia mambo makuu, anaendeleza uzazi, anawakilisha watu wengine katika jamii. Ni kama mti uliomo kando ya mto wa kulisha jamii, ni baba ya mayatima, analinda mali, anawalinda wanyonge, ana msimamo, ni mwenye hekima na hana mapendeleo.

Kuna wimbo mmoja ulioimbwa na msanii maarufu wa jamii ya Kalenjin marehemu Kipchamba Arap Tapotuk, ulioeleza kwamba mwanaume hapaswi kusikia maneno ya mwanamke kwani maneno yao hutoka kwenye akili ya kushoto ilhali ya mwanaume hutoka upande wa kulia. Maneno ya mwanamke yakisikilizwa, yatakosanisha watu katika jamii. Kupitia wimbo huu, imedhihirika kwamba hadhi ya mwanamke imeshukishwa na ya mwanaume imeinuliwa. Wakati wa kampeni, mwanaume anahimizwa kwamba akipata uongozi afuate mkondo fulani wa uongozi ambao mwanaume mashuhuri wa awali aliutumia.

Mwanaume anafananishwa na watu mashuhuri wapatikanao katika Biblia takatifu. Anafananishwa na Musa aliyegonga maji ya Bahari Nyekundu akitumia fimbo hadi maji yakatawanyika kisha Wayaudi wakavuka. Anafananishwa na Yusuf alipokuwa Misri ambaye aliwalisha watu wake wakati wa njaa kali. Kulingana na nyimbo hizo, inambidi mwanaume abarikiwe na wazee wa jinsia ya kiume namna mwana wa Jesse alibarikiwa kama tuelezwapo katika Biblia. Kuambatana na Ubabedume ambao umekithiri na kukolea katika akili za watu katika jamii, mwanaume anaonekana kana kwamba anastahili kutawala.

Kulingana na nyimbo hizo za kampeni za kisiasa, mwanamke hasawiriwi kuwa na uwezo mkubwa wa kutawala. Sifa zake zidhihirishwazo si za nguvu za kimwili ama za misuli. Wasanii wa nyimbo walikuwa wakimtetea wakieleza kwamba yeye anaweza kuwa kiongozi kwa sababu yeye ni mama. Yeye ana uwezo wa kulisha jamii, ana upendo, ni mwenye huruma, ni mnyenyekevu, mpole, mtulivu, mwaminifu, mkarimu na ni mtunzaji wa nyumbani kwake. Mama huletea jamii maendeleo makubwa kila mara daima kwani yeye ni mwaminifu. Mwanamke anaweza kufanya mambo makuu yeye mwenyewe bila usaidizi wa mwanaume kwani hata anaweza kwenda vitani mwa kisiasa na kuwa mshindi. Vilevile, nyimbo zilieleza kwamba hakuna kitu kinachofananishwa na mama. Nyimbo nyingine zilitetea haki za mwanamke kwa kueleza uwezo wao. Nyimbo hizo zilifahamisha kwamba kumekucha na tunataka mabadiliko kuhusu jambo hili katika masuala ya kisiasa, kijamii, kiuchumi na kifikra. Katika jamii ya Kalenjin, wanawake na watoto hujumlishwa kuwa sawa lakini ni wazi kwamba jambo kama hili limepitwa na wakati kuambatana na maelezo tuliyoyapata katika nyimbo za kampeni za kisiasa kuhusu jinsia ya kike. Jambo hili lilikuwa likitendeka ili mwanamke apate kuongozwa, kutawaliwa na kuelekezwa pamoja na watoto bila yeye kuteta.

Utafiti huu umefanikiwa kuonyesha kwamba nyimbo nyingi ziliunga mkono taasubi za kiume. Kwa kueleza kwamba mwanaume ni mfano wa moto, anaweza kumwua simba anayenguruma au hukinga pembeni, husawiri ujasiri, nguvu na uwezo wake mwingi. Hizi ni sifa hasa za kimwili zihitajikazo katika jambo gumu kama vita. Kwa sababu nyimbo hizi zilikuwa zikilenga siasa, inamaanisha kwamba siasa yenyewe imefananishwa na vita na kwa hivyo inahitaji mtu

mwenye sifa kama hizi. Mwanamke hawezi kuhusishwa na sifa kama hizi katika jamii. Hapo ndipo mwanaume atapata nafasi ya kupanda ngazi kisiasa akijilimbilizia mali. Mwanamke hajapewa nafasi ya kutosha na jamii kufikia kiwango hicho. Matokeo haya yanadhihirisha kwamba jamii inakuza na kuendeleza ubabedume.

**MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

**Mahitimisho:** Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kwamba maudhui ya nyimbo za kampeni za kisiasa husawiri historia, itikadi na mielekeo ya jamii kuhusu jinsia ya kike na ya kiume. Kulingana na nadharia ya Ubabedume, kiutamaduni, wanaume hufundishwa katika jamii wawe viongozi hasa wa wanawake. Kimmel (1997) akinukuliwa na Aswani na wengine (2014), aeleza kwamba nadharia ya Ubabedume hufafanua sifa mahususi anazostahili kuwa nazo mwanaume. Kuambatana na namna jinsia imewakilishwa katika nyimbo za kampeni za kisiasa, wagombezi wa kiume waliogombea viti mbalimbali vya kisiasa walikuwa wengi kuliko wa kike. Jambo hili linadhihirisha kuwa ubabedume umedumishwa katika jamii ilhali ubabejike bado unajitafutia nafasi kwa umbali. Vilevile, wasanii walieleza kuhusu maendeleo yaliyofanywa na wagombezi wa kiume waliotaka kuwania viti vya kisiasa tena. Hii ni njia moja ya kuendeleza utawala wa wanaume. Wanawake bado wananyimwa nafasi ya uongozi kisiasa katika jamii ambapo itikadi inayotawala inawakuza wanaume.

**Mapendekezo:** Kwa kuzingatia matokeo hayo, mtafiti apendekeza kwamba wasanii wahamasishwe wabuni na kuwaimbia wanawake nyimbo za kuwaunga mkono na kuwapa motisha katika siasa jinsi wanaume wanavyoimbiwa. Pia, apendekeza kuwa wasanii wa jinsia ya kike wahimizwe kuimba nyimbo za kisiasa wakilenga wagombezi wa kike ili kuwapa moyo kwani wanawake kwa wanawake huelewana.

**MAREJELEO**


Aswani, B., Mayaka, G., & Riro, M. (2014). *Misingi ya Nadharia na Mbinu za Utafiti.* Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

Carrigan, T., Connel, R., & Lee, J. (1985). Toward a New Sociology of Masculinity. In H. Brod Editor. *The Making of Masculinities. The New Men Studies*.

Commonwealth Observer Group. (2013). *Report of the Commonwealth Observer Group*. Kenya General Elections.

Connell, R. (1983). *Which Way is Up*. Sage Publications.

Connell, R. (1987). *Gender and Power: Society, the Person and Sexual Politics.* Sage Publications.

DDDG. (1998). *Final Report*: Kenya General Elections 1997 (The Donors' Democratie Development Group).

Kimmel, M. (1997). Masculinity as Homophopia: Shame and Silence, in Harry Brod and Micharel Kaufam. *Theorizing Masculinities*. Sage Publications.

Maclenness, J. (1998). *The End of Masculinity.* Open University Press.

Mazrui, A. M., & Syambo, B. K. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. East African Educational Publishers.

Richmond, A. M. (1992). *Masculine and Feminine: Gender Roles Over the Life Cycle*. (i): Sage Publications.

Riordan, L. (2007). *The American Revolution and its Legacy in the Mid-Atlantic.* University of Pennsylvania Press.

Sengo, T. S. Y., & Kiango, S. D. (1973). *Hisi Zetu.* 1. TUKI.

Smith, J. E. (2012). *Eisenhower in War and Peace*. Random House.

Uchendu, E. (2005). *Masculinities from Perspectives of Youth.* Paper Presented at the Gender Institute-CODERSIA.

Wafula, R. M., & Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Jomo Kenyatta Foundation.